MATUNDASI ASM DEVELOPMENT COMPANY LIMITED
https://www.matundasiasm.co.tz/ info@matundasiasm.co.tz

**28 Mei, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Matundasi ASM Development Company Limited (MADC) ni kampuni inayojishughulisha na utafiti na uchimbaji wa madini katika Mkoa wa Mbeya, wilaya ya Chunya. Kampuni hii inawatangazia wote wenye sifa tajwa kuwasilisha maombi ya kuajiriwa katika nafasi mbalimbali kama ifuatavyo:

## MADEREVA WA MALORI (Truck Drivers)

### DEREVA MWANDAMIZI WA MALORI (Senior Truck Driver) – Nafasi Mbili (02)

**SIFAZA MUOMBAJI**

- Diploma katika fani za udereva au ufundi wa malori au vyote.
- Uzoefu usiopungua miaka 10 katika udereva wa malori na usimamizi wa madereva wengine.
- Uzoefu wa kuendesha aina mbalimbali za malori.
- Uelewa wa msingi wa mitambo ya malori kwa ajili ya kutoa taarifa za matatizo ➢ Uzoefu wa kusimamia au kuongoza timu ya madereva.
- Uwezo wa kuendesha malori kwenye nchi jirani na Tanzania.
- Uwezo wa kuendesha malori yenye tela au vifaa maalum.
- Uelewa wa kanuni za usalama barabarani na mbinu za udereva wa kujihami.
- Leseni halali ya udereva (Daraja E) kutoka chuo cha udereva kinayotambulika.
- Cheti cha usalama au udereva wa kujihami (defensive driving course) kutoka LATRA kitahesabiwa kama sifa ya ziada.
- Uwezo wa kutatua matatizo, kupanga shughuli, na kudumisha mawasiliano mazuri kazini.
- Uwezo wa kuandaa ripoti za kila siku na kila mwezi za magari yote ➢ Umri usiozidi miaka 45.

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**

- Maombi yaelekezwe kwa:
  **Afisa Rasilimali Watu**
  Matundasi ASM Development Company Limited,
  S.L.P 70812,
  DAR ES SALAAM,
- Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe info@matundasiasm.co.tz na hr@matundasiasm.co.tz
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20 Juni, 2025**, na kichwa cha barua pepe kiwe jina la nafasi unayoomba.

**VIAMBATANISHO MUHIMU**

- Waombaji wenye sifa wanatakiwa kuwasilisha barua ya maombi ikiwa na nyaraka zifuatazo:
    a) Nakala za vyeti husika (vilivyothibitishwa),
    b) Nakala ya leseni
    c) Nakala ya cheti Cha utumishi (kampuni aliyotoka)
    d) Picha mbili (2) za pasipoti za hivi karibuni,
    e) Wasifu binafsi (CV)
    f) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
    g) Police Fingerprint.
    h) Wadhamini watatu (wa nje na ndani ya familia ikiwa na picha za wadhamini na anuani zao (nambari za simu)
    i) Barua ya wadhamini watatu, mmoja (01) wa nje na wawili (02) wa familia pamoja na picha(passport) zao na mawasiliano yao yanayopatikana.
    j) Barua ya utambulisho kutoka serikali za mtaa anapotokea.
- Waombaji waliotimiza vigezo ndio watakaoitwa kwa ajili ya usaili.

MATUNDASI ASM COMPANY LTD